# Serikali kujenga bwawa la kunyweshea mifugo Liwale

**Na Mwandishi Maalumu, Liwale**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema katika bajeti ya mwaka 2021/2022 serikali itajenga bwawa la kunyweshea mifugo lenye thamani ya Sh milioni 480 katika Kijiji cha Kimambi wilayani Liwale, Lindi.

Ulega aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika Wilaya ya Liwale mkoani Lindi iliyolenga kusikiliza kero za wafugaji na wakulima ili kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo utasaidia kutatua changamoto ya maji ambayo inawakabili wafugaji wa maeneo hayo na kwamba utasaidia pia kutatua migogoro baina yao na wakulima wilayani humo.

"Rais Samia Suluhu Hassan anakwenda kuwajengea bwawa lenye thamani ya shilingi milioni 480 hapa Kimambi, ujenzi wa bwawa hilo utasaidia kuwaondoa katika migogoro," alisema Ulega.

Ulega aliwataka viongozi wa wilaya hiyo kuhakikisha pesa hizo zinatumika vizuri kwa shughuli iliyokusudiwa na si vinginevyo.

Aidha, alisema Rais Samia amewapa pia majosho mawili katika Kijiji cha Kimambi na Kijiji cha Luwele.

"Sasa kwa sababu huku mifugo imekuwa mingi sana, mimi nakuongezeeni josho lingine hapa ili mifugo mingi iweze kuogeshwa," aliongeza.

Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka, alitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais Samia kwa kuwapa pesa za kujenga bwawa na kuongeza kwamba bwawa hilo likikamilika hawatarajii tena kuona migogoro katika vijiji vilivyotengwa kwa ajili ya wafugaji wilayani humo.

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 15

# Wavuvi nchini kupewa vitambulisho

Na Alexander Sanga, Mwanza

WAVUVI nchini wanatarajiwa kupewa vitambulisho ili watambulike.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti wa Chama cha Wavuvi nchini (TAFU), Bakari Kadabi, wakati wa kikao cha wadau wa uvuvi kuhusu mikakati ya kupambana na uhalifu ndani ya Ziwa Victoria.

"Tutaanzisha umoja wa wavuvi katika kila eneo na hii itasaidia sana kuwatambua wavuvi wote pamoja na kuwapa vitambulisho,'' alisema.

Alisema moja ya vikwazo vikubwa kwa wavuvi ni matukio ya wizi wa mashine za mitumbwi pamoja na nyavu, jambo ambalo alisema wanaendelea kupambana nalo.


Alisema kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi nchini wataendelea kufuatilia kwa lengo la kujua mashine na nyavu zinazoibiwa zinaenda kuuzwa wapi.

Kwa upande wake, Kamishina wa Polisi na Mafunzo, Liberatus Sabas, alisema tofauti na zamani, kwa sasa matukio ya uhalifu katika Ziwa Victoria yamepungua.

"Uhalifu umepungua kutokana na jitihada kubwa zilizofanyika kwa muda mrefu. Miaka ya nyuma kwa siku kulikuwa kunaripotiwa matukio matatu hadi manne ya unyang'anyi ndani ya ziwa lakini kwa sasa tunapokea wastani wa tukio moja kwa mwezi," alisema Sabas.

Aliwataka wadau mbalimbali kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi nchini kuhakikisha wanatokomeza kabisa uhalifu katika Ziwa Victoria.

"Ziwa Victoria ni chanzo kikubwa cha mapato cha mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla, kwa hiyo sisi Jeshi la polisi tutaendelea kulinda ziwa hili... Mara kadhaa tunapata taarifa kuwa uhalifu unafanywa na watu kutoka nchi za jirani," alisema Sabas na kuongeza kwamba, wanaendelea kuandaa mikakati endelevu ili kumaliza kabisa uhalifu katika ziwa hilo.



Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT), James Mbulwe (wa pili kushoto) akimkabidhi Mkurugenzi wa taasisi ya Population Priority Service, Isack Kalumba mfano wa hunndi ya Sh milioni 3.4 kwa ajili ya kupanda miti mkoani Dodoma. Hafla iliyofanyika mkoani Dar es Salaam juzi. Bodi hiyo pia ilikabidhi Sh milioni 2 kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sh milioni 1.5 kwa Chama cha wasioona Temeke, Sh milioni 1.7 kwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu Dar es Salaam kwa ajili ya kununua vifaa vya elimu. Wanaoshuhudia ni maofisa wa Bodi hiyo, Catherine Lamwai (kushoto) na Sadiki Elimsu (Picha na Yusuf Badi)

# Serikali kujenga bwawa la kunyweshea mifugo Liwale

Na Mwandishi Maalumu, Liwale

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema katika bajeti ya mwaka 2021/2022 serikali itajenga bwawa la kunyweshea mifugo lenye thamani ya Sh milioni 480 katika Kijiji cha Kimambi wilayani Liwale, Lindi.

Ulega aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika Wilaya ya Liwale mkoani Lindi iliyolenga kusikiliza kero za wafugaji na wakulima ili kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo utasaidia kutatua changamoto ya maji ambayo inawakabili wafugaji wa maeneo hayo na kwamba utasaidia pia kutatua migogoro baina yao na wakulima wilayani humo.

"Rais Samia Suluhu Hassan anakwenda kuwajengea bwawa lenye thamani ya shilingi milioni 480 hapa Kimambi, ujenzi wa bwawa hilo utasaidia kuwaondoa katika migogoro," alisema Ulega.

Ulega aliwataka viongozi wa wilaya hiyo kuhakikisha pesa hizo zinatumika vizuri kwa shughuli iliyokusudiwa na si vinginevyo.

Aidha, alisema Rais Samia amewapa pia majosho mawili katika Kijiji cha Kimambi na Kijiji

# Bodi ya kahawa yapambana kuongeza uzalishaji maradufu

Na Upendo Mosha, Moshi

wakati akitoa taarifa

"Tuna mpango wa ku-

maofisa kilimo pamoja

Scanned with CamScanner



UHURU UK 9.

# Watuhumiwa 19 wanaswa Rorya wizi wa mifugo

**Na MWANDISHI WETU,** Tarime

POLISI Kanda Maalumu ya Tarime na Rorya, imewakamata watuhumiwa 19 wanaodaiwa kujihusisha katika matukio ya wizi wa mifugo.

Pia, imekamata gari aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili T 450 CSJ ambalo limeondolewa viti vya ndani linalodaiwa kutumika kusafirishia mifugo.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Kanda ya Tarime na Rorya, ACP William Mkonda, alisema kuanzia Septemba 11, mwaka huu, wamekuwa wakifanya msako dhidi ya watu wenye mtandao wanaojihusisha na wizi wa mifugo.

"Kati ya watuhumiwa hao 19, watatu wanahusika katika kusafirisha mifugo kwa kutumia gari aina ya Hiace lenye namba ya usajili T 450 CSJ ambalo mmiliki wake yupo Sirari mpakani.

"Watuhumiwa 12 ni wezi wa mifugo, saba kati yao ni wezi sugu waliotoka magerezani kati ya Aprili na Julai mwaka huu.

"Tumefanikiwa kuokoa ng'ombe 29 waliokuwa wameibwa kutoka vijiji mbalimbali vya wilaya za Tarime na Rorya.

"Polisi tunatoa wito kwa jamii kuendelea kutoa ushirikiano na taarifa kwa kuwafichua wezi wa mifugo waliopo katika maeneo yenu ili waweze kukamatwa popote walipo," alisema kamanda huyo.

regions.

For his part Mahmoud said cooperation in supervision of

Some MPs by the speak with the resi projects thr Funds.

Member said MPs h existing ch social and

Oldonyowas Secondary School students Linda Joseph (2nd-L) and Venancia Julius demonstrate their 'wizardry' in Biology and Chemistry to Arusha City Council officials on a tour of the school at the weekend. Photo: Correspondent Woinde Shizza

THE GUARDIAN Page 3.

# *Govt to build 480 million/- worth* dam for herders in Liwale District

**By Guardian Reporter, Liwale**

DEPUTY Minister for Livestock and Fisheries Abdallah Ulega has said that in its FY 2021/22 budget, the government will construct a water dam for livestock, expected to cost 480m/- at Kimambi Village in Liwale District, Lindi Region.

He made the remarks on Monday this week during his visit in Liwale District to listen to complaints from livestock keepers and farmers.

He said the construction of the dip will help to solve water challenges faced by herders for their animals as well as finding solution to conflict pitting between livestock keepers and farmers in the district.

Ulega stressed that the funds provided will be spent on the dam to provide water for livestock and called on district officials to make sure the money is well spent.

He added that the government has also constructed two cattle dips at Kimambi and Liwale districts.

For his part, Liwale Member of Parliament, Zuberi Kuchauka used the occasion to thank President Samia Suluhu Hassan for setting aside the funds saying when completed, the water dam will see the end of conflicts in the villages set aside for herders in the district.

Scanned with CamScanner